Ecolebooks.com

Mtihani wa pamoja
Muhula wa pili –
Kidato cha pili

Mwongozo wa kusahihisha

1. **Kipe kifungu hiki kichwa mwafaka.** **(ala.1)**
   Wanawakiwa/ Mateso ya wanawakiwa 1x1 = 1mks
2. **Eleza dhana ya 'Mwanamkiwa.** **(ala. 1)**
   Ni Yule yaliyefiwa na mzazi mmoja au wote wawili
3. **Ni kategoria gani ya wanawakiwa inayosumbuka sana?** **(ala. 2)**

Ni watoto wanahitaji kulelewa na kupewa matakwa ya kimsingi kama chakula, mavazi, malazi elimu n.k 1x 2 = 2

4. **Taja mambo mawili ambayo baadhi ya imani na mila za jadi huchukulia kuwa chanzo cha uanaukiwa.** **(ala.1)**

i) Laana 2x 1 = 2
ii) Urogi

5. **Eleza kwa kifupi hali ya elimu ya wanawakiwa.** **(ala.2)**
   i) Baadhi ya walioachiwa wanawakiwa huwaelimisha
   ii) Wengine huwanyima hata elimu hivyo baadhi yao kutojua kusoma na kuandika.
6. **Taja mateso mawili ambayo wanawakiwa wanaoahidiwa kulepekwa ng'ambo hukumbana nayo.** **(ala.2)**

   i)_Kushikwa shokoa

   ii) Kutumiwa kama vyombo vya kuuza madanguroni 2x 1= 2mks)

7. **Eleza unafiki wa baadhi ya watu wa jamii ya wanawakiwa.** **(ala.3)**

i) Kujitia wana huruma mzazi afapo.
ii) Kuishia kuwatesa wanawakiwa
iii) Huwapeleka ng'ambo wanakoteswa 3x1 = 3mks)

8. **Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika makala.** **(ala.3)**
   i) **Inakela –** Sumbua

      - Fanya jambo la karaha au kuleta uchukivu

   ii) **Waja –** wanadamu/watu/adinasi/insi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

a) Ni sababu zipi zinazosababisha umaskini wa wanawake wa shambani? (Maneno 5-55)

Jibu

i) Mazingira magumu
ii) Wanabaguliwa na sera nautamaduni
iii) Wanakumbana na matatizo kama viongozi wa miji
iv) Hawapati usaidizi
v) Hawana nafasi ya kushiriki katika maamuzi
Alam 5
Mtiri 2

b) Eleza jinsi wanawake wa mashambani wanavyoathirika vibaya(maneno 40 – 45)

Jibu

i) Umaskini unaotokana na ongezeko la watu
ii) Matatizo ya kiuchumi ulimwenguni
iii) Majanga ya kiasilia
iv) Uharibifu wa mazingira
v) Kuvunjika kwa familia
vi) Ukosefu wa mikakati ya kupambana na hali alama 6 mtiririko 2

Sarufi na matumizi ya lugha. *(ala. 40)*

a) Eleza sifa mbili za sauti|k|. (ala.2)

Ni kipasuo

Ni sauti si ghuna

b) Andika mfano mmoja wa neno lenye muundo ufuatao: (ala.1)
IKII

-Okoa

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

-Itia
-Elea
-Ozea

c) Sentensi ambatano ni ipi? (ala. 2)

Ni sentensi iliyoundwa kutokana na sentensi mbili sahili au zaidi zilizounganishwa kwa viunganishi

d) Unda sentensi yenye muundo ufuatao. (ala.2)
W+V+T+E
Yule mzuri amepita sana

e) Onyesha viwakilishi (w) katika sentensi ifuatayo na ueleze ni vya aina gani. (ala.2)
Wote walipewa kile kizuri.

i)wote – w- cha pekee
ii) Kile – w (kionyeshi/ kiashiria)

f) Yakinisha sentensi ifuatayo. (ala. 1)
Hakula akashiba.
- Alikula akashiba

g) Kanusha sentensi ifuatayo. (ala.2)
Ningeenda kwake leo angenipa mawaidha.
-Nisingeenda kwake leo asingenipa mawaidha.

h) Eleza dhana zinazojitokeza katika maneno yaliyopigiwa mstari. (ala.3)
Mtoto <u>mwenye</u> tabia nzuri ni Yule.
Mwenye – dhana ya ‘kuwa na’ ‘ kumiliki’
Mtoto <u>mwenyewe</u> alianguka <u>mle</u>
Mwenye – dhana ya ‘kuwa na,’ ‘kumiliki’
Mle – dhana ya mahali ndani
Mle – dhana ya kiashiria cha umbali

i) Tunga sentensi kuonyesha vielezi vifuatavyo. (ala.3)
a) Kielezi cha wakati
- Tulienda nyumbani jana
b) Kielezi cha mahali
- Kamau alienda nje
c) Kielezi cha namna/jinsi
- Waliandika insha <u>vizuri</u>

j) Andika katika msemo halisi. (ala. 2)

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Rafiki yetu alitujulisha kuwa tungeondoka siku iliyofuatia kuelekea Afrika kusini.
"Mtaondoka kesho kuelekea Afrika kusini."
Rafiki yetu alitujulisha.

k) Unda nomino kutokana na maneneo yafuatayo. (ala. 3)

Neno		Nomino
i)	Fikiri	fikra
ii)	- la	mlo, chakula, ulaji, mlaji
iii)	Kubwa	ukubwa

l) Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina zifuatazo za nomino. (ala. 2)

i) Nomino kitenzi – jina
Kucheka huko kunaudhi.

ii) Nomino dhahania
Ukali wake ulimfanya aogopwe

m) Onyesha vivumishi (v) kwa kupigia mstari na ueleze ni vya aina gani. (ala.2)
Waziri wa kawi anaishi katika nyumba kubwa.
V 'wa' cha a- unganifu
V 'kubwa' cha sifa

n) Tumia alama ya ritifaa katika sentensi kuonyesha matumizi mawili tofauti. (ala. 2)

-Ng'ombe atachinjwa

-Tutapika s's' hivi.

-Taralamu iliyoachwa km mwaka wa is.

o) Bainisha viambishi katika neno lifuatalo. (ala.3)
Waliotutenga
wa – nafsi
li – wakati
o – kirejeshi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

tu – watendwa
teng - Mzizi wa kitenzi
a - kiishio

p) Nyumbua vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa. (ala.6)

Kitenzi	tendesha	tendeshea
Piga	pigisha	pigishia
-la	lisha	lishia
-nywa	nywesha	nyweshea

q) Mahali palipotayarishwa pamejaa wageni kutoka mbali. (Anza kwa: wageni…)al.2)

- Wageni kutoka mbali wamejaa mahali palipotayarishwa

IV ISIMU – JAMII

Mtu X : wauza how much?
Mtu Y: Hamsini kastoma.
Mtu X: Kumbe ni expesive hivyo?
Mtu Y: Nitakupunguzia. Toa arobaini.
Mtu X: Haya. Nipatie change.

a) Hii ni sajili gani? (ala.1)

-sokoni

b. Eleza sifa tano za sajili hii. (ala5)

i) Ni lugha isiyo rasmi
ii) Lugha ya kuchanganya ndimi
iii) Ina – matumizi ya utohozi

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

iv) Huwa ni lugha ya mazungumzo ya kitamthilia
v) Ina ushawishi mwingi
vi) Msamiati maalum unaohusiana na biashara mf. ngapi, expensive, kastoma

Taja athari mbili hasi za lugha ya 'Sheng' (ala.2)

i) Kushindwa kuzungumza lugha sanifu hasa katika mazingira rasmi.
ii) Huchangia makosa ya kisarufi
iii) Ni vigumu kujifunza lugha sanifu
iv) Wazungumzaji huenda wasielewane.

b) Kwa nini vijana hutumia lugha ya 'Sheng' Eleza sababu mbili. (ala.2)

c) Kutaka kuwa ni siri katika mazungumzo
d) Kutaka kujitambulisha na kundi fulani
e) Kurahisisha mazungumzo yao
f) Kuhisi kuwa ni mabingwa katika kubuni msamiati mpya.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM